TANGAZO LA SERIKALI NA. 98 la tarehe 17/03/2017

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
SURA 290

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA MUSOMA ZA MWAKA, 2017

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Musoma za mwaka, 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Musoma.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:-

“Ada na Ushuru” maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

“Afisa masuuli” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au afisa yeyote atakaye idhinishwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

“Afisa Mwidhiniwa” maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

“Bidhaa“ maana yake ni kitu chochote chenye thamani kilicholetwa sokoni au gulioni kwa lengo la kuuzwa.

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya Musoma.

“Kibali’ maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.

“Leseni” maana yake ni kibali cha maandishi kinachotolewa kwa Mtu binafsi, Kampuni au taasisi kinachoruhusu kufanya biashara au shughuli yoyote katika eneo la Halmashauri.

"Machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi.

"Masoko" maana yake ni sehemu maalumu iliyotengwa na kumilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya biashara ya kuuza na kununua bidhaa au huduma kufuatana na taratibu zilizowekwa na Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Musoma pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mkataba" maana yake ni makubaliano yenye nguvu ya kiSheria ya ununuzi au uuzaji au utoaji wa huduma yoyote kati ya Halmashauri na mdau husika.

"Wakala" maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni au asasi yoyote iliyoteuliwa kiSheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

Ada na Ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru katika biashara, huduma, vibali, au leseni mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoorodheshwa kwenye jedwali la kwanza Sheria Ndogo hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla kifungu kidogo cha (1 ) cha 4 cha Sheria Ndogo Halmashauri itatoza Ada na Ushuru katika vyanzo vifuatavyo:-

i. Ushuru wa Kupakia na Kupakua Bidhaa
ii. Kibali cha Kusafirisha bidhaa
iii. Ada ya Maegesho ya mitumbwi na boti
iv. Ada ya maombi ya kuchimba/kupitisha mtaro kwenye eneo la barabara
v. Ada ya Mabango
vi. Ada ya Shughuli za Utamaduni.
vii. Ushuru wa machinjio na ada ya ukaguzi wa nyama.
viii. Adaya vibali vya ujenzi

Namna ya kukusanya Ada na Ushuru

5 (1) Halmashauri itaweka utaratibu itakavyoona inafaa ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo maalum ya kutoza Ada na Ushuru kutoka vyanzo vya mapato kama ilivyoainishwa kwenye kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo hizi.

(2) Malipo ya Ada au Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au wakala na kutolewa stakabadhi halali ya kielektroniki kama

kielelezo cha malipo yaliofanyika.

(3) Ada na Ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupata huduma, leseni au kibali husika.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 5 cha Sheria Ndogo hizi Halmashauri au wakala kwa idhini ya Afisa Masuuli itatoa kwa mlipaji stakabadhi halali ya kawaida kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika endapo stakabadhi ya kielektroniki haiwezi kutolewa.

(5) Halmashauri au Wakala atakuwa na mamlaka ya kukamata bidhaa au mali ya mtu yeyote endapo ameshindwa kulipa Ada au Ushuru ndani ya muda aliotakiwa kulipa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(6) Endapo bidhaa au mali iliyokamatwa na Halmashauri au wakala haitalipiwa Ada au Ushuru unaodaiwa ndani ya siku 7 kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka, na ndani ya siku 2 kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuuza bidhaa au mali na fedha zitakazopatikana zitawekwa kwenye akaunti ya Halmashauri

(7) Wakala hataruhusiwa kuuza au kufanya jambo lolote kwa mali au bidhaa iliyokamatwa bila kupata idhini ya Afisa Masuuli.

Wajibu wa kulipa Ada au Ushuru

6 (1) Ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada au Ushuru kulipa kiwango cha Ada au Ushuru kama ilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni wajibu kwa kila mtu kutoa taarifa sahihi kwa Halmashauri au Wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.

(3) Itakuwa ni wajibu kwa kila mtu atakayelipa Ada au Ushuru kutunza kumbukumbu za malipo.

Kibali au leseni

7. (1) Halmashauri itatoa kibali au leseni kwa mfanyabiashara au mtu yeyote kwa kadri itakavyoona inafaa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni wajibu kwa kila mfanyabiashara au mtu yeyote anayetaka kufanya jambo lolote linalohitaji kibali au leseni kuomba na kupata leseni au kibali kutoka Halmashauri.

Uteuzi wa wakala

8. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua Kampuni au Taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria kukusanya Ada au Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa wakala

9. Wakala aliyeteuliwa chini yakifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:

(a) Kukusanya na kupokea Ada au Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alililopangiwa na kwa kiwango kilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

(b) Wakala atakusanya Ada au Ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Makosa kwa Wakala

10. Itakuwa ni kosa kwa Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo:-

(1) Atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataa kulipa Ada au Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi.

(2) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada au Ushuru.

(3) Atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(4) Atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada au Ushuru ndani ya halmashauri

(5) Atashindwa au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.

(6) Atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya Ada au Ushuru.

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi Shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungu kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja na kulipa fedha anazodaiwa.

Uwezo wa Afisa mwidhiniwa

11. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote au jengo lolote kwa nia ya kukusanya au kufanya tathimini au kufanya jambo lolote linalohusiana na Ada, Ushuru, leseni au Kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa

12. Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mtu yeyote:-

1) atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataa kulipa Ada au Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na

halmashauri kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi.

2) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada au Ushuru.
3) atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.
4) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada au Ushuru ndani ya halmashauri.
5) atashindwa kutoa taarifa sahihi au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.
6) atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya Ada au Ushuru.

Kufifilisha Makosa

13. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria hizi, kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini (Tsh.50,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi, na atatakiwa kulipa Ada na Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

14. Mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa, na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (Tsh.50, 000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

Kufutwa kwa Tangazo la Serikali

15. 1. Sheria Ndogo hizi zinafuta sheria Ndogo zifuatazo:-

GN.No. 202/2009

(i) Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Musoma ‘Fees and Charges’ za mwaka 2009;

GN.No. 153/2013

(ii) Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Musoma (Kibali cha Ujenzi), 2013;

GN.No. 159/2013

(iii) Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Musoma (Ada ya Shughuli za Kiutamaduni), 2013;

GN.No. 193/2009

(iv) Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Musoma (Ushuru wa Maegesho ya Vyombo vya Majini), 2009 zimefutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Chini ya kifungu cha 4 (1)*

SEHEMU YA KWANZA

USHURU WA KUPAKIA NA KUPAKUA BIDHAA

BIDHAA ZA MAJINI

| | |
|---|---|
| Kilo moja ya samaki wabichi | 5% ya bei ya soko/ununuzi |
| Tenga dogo la samaki wakavu Kg 0-20 | Halilipiwi |
| Tenga la saizi ya kati la samaki wakavu Kg 21-50 | 5,000/= |
| Tenga kubwa la samaki wakavu Kg 51-100<br><br>Kwa kila kilo inayoongezeka zaidi ya Kg 100 | 10,000/=<br><br>500/= |
| | |
| Gunia la dagaa lenye Kg 0-10 | Halilipiwi |
| Gunia la dagaa lenye Kg 11-50 | 3,000/= |
| Gunia la dagaa lenye Kg 51-100<br><br>Kwa kila kilo inayoongezeka zaidi ya Kg 100 | 5,000/=<br><br>500/= |
| | |

Gunia la magamba ya konokono:

| | |
|---|---|
| Kg 1-20 | 1,000/= |
| Kg 21-50 | 2,000/= |

| | |
|---|---|
| Gunia la mabondo Kg 1-20 | 30,000/= |
| Gunia la mabondo Kg 21-50 | 100,000/= |
| Gunia la mabondo Kg 51-100<br><br>Kwa kila kilo inayoongezeka zaidi ya Kg 100 | 150,000/=<br><br>30,000/= |

Chakula cha mifugo:

| | |
|---|---|
| Gunia lenye kg 1-20 | Halilipiwi |
| Gunia lenye kg 20-50 | 2,000/= |
| Gunia lenye kg 51-100<br><br>Kwa kila kilo inayoongezeka zaidi ya Kg 100 | 3,000/=<br><br>500/= |
| Mabini ya samaki | 20,000/= kwa mwezi |
| | |

BIDHAA ZA KILIMO

| | |
|---|---|
| Pamba | 5% ya bei ya shambani au itakayoamriwa na bodi ya pamba |

| | |
|---|---|
| Mahindi…Gunia Kg 20- 100<br><br>zaidi ya Kg 100 | 1,500/=<br><br>3,000/= |
| Mpunga…Gunia Kg 20-100<br><br>zaidi ya Kg 100 | 1,000/=<br><br>3,000/= |
| Mihogo/makopa/viazi………Gunia Kg 20-100<br><br>zaidi ya Kg 100 | 1,000/=<br><br>1,500/= |
| Ulezi/uwele/mtamaGunia Kg 20-100<br><br>zaidi ya Kg 100 | 1,500/=<br><br>3,000/= |
| Maharage/jamii ya maharage…. Gunia Kg 20-100<br><br>zaidi ya Kg 100 | 1,500/=<br><br>3,000/= |
| Maembe………Gunia Kg 20-100<br><br>zaidi ya Kg 100 | 3,000/=<br><br>5,000/= |
| Alizeti……………… Gunia Kg 20-100 | 3,000/= |
| Mchele……… Gunia la Kg 25-50<br><br>Kg 50-100 | 1,500/=<br><br>3,000/= |
| Mkungu wa ndizi | 500/= |
| Mzigo wa Miwa | 1,000/= |
| Nyanya tenga la debe 3<br><br>zaidi ya debe 3 | 3,000/=<br><br>5,000/= |
| Vitunguu Gunia la Kg 20-100<br><br>zaidi kg 100 | 3,000/=<br><br>5,000/= |
| Karanga Gunia la Kg 50-100<br><br>zaidi ya Kg 100 | 5,000/=<br><br>500/= @ Kg |
| Tikiti Maji ........ Tani 0-1<br>zaidi ya Tani 1 | 5000/=<br>2000/= @ Tani |
| Mazao mengine ambayo hayajabainishwa... Gunia/tenga kg 20-100<br><br>zaidi kg 100 | 1,000/=<br><br>2000/= |

BIDHAA ZA VIWANDANI

| | |
|---|---|
| Gari la bidhaa za viwanda la tani 1- 9 | 5,000/= |
| Gari la tani 10 na zaidi lenye bidhaa za viwandani lenye 'trailer' | 15,000/= |
| Gari la tani 10 na zaidi lenye bidhaa za viwandani lisilo na ' tlailer' | 10,000/= |
| Robota ''Ballon'' la mitumba | 3,000/= |
| Gari la mafuta ya taa, au diesel, au petrol chini ya tani 10 | 10,000/= |
| Gari la mafuta ya taa, au diesel, au petrol zaidi ya tani 10 | 15,000/= |
| Gari la gesi na bidhaa nyingine za mlipuko chini ya tani 10 | 20,000/= |
| Gari la gesi na bidhaa nyingine za mlipuko zaidi ya tani 10 | 30,000/= |

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI

Kibali cha kusafirisha bidhaa kutoka katika halmashauri ya wilaya ya musoma
Kibali kinatolewa kwa Ndugu……………………………………………………………………….
Mmiliki wa Leseni yenye Na……………………………….. toka ………………………………….
Kwa ajili ya kusafirisha bidhaa toka Halmashauri ya Wilaya ya Musoma kwenda …………………
Kwa bidhaa yenye maelezo yafuatayo:

| Aina ya bidhaa inayosafirishwa | Idadi/Ujazo wa mzigo | Ada na Ushuru uliolipwa Halmashauri | Na. ya risiti | Mahali bidhaa inapopelekwa | Tarehe ya kusafirisha bidhaa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

Kibali cha kusafirisha bidhaa hizi kimetolewa leo hii tarehe………..mwezi……….mwaka………..

Jina la Afisa mhidhiniwa……………………

Sahihi………………….

Cheo……………………

Jina la mwombaji wa kibali………………………

Sahihi……………………..

Tarehe…………………….

SEHEMU YA PILI

ADA YA MAEGESHO YA MITUMBWI NA BOTI

| | |
|---|---|
| Mtumbwi | 1000 kwa siku |
| Kalua/Ngama | 6000 kwa siku |
| Kivuko 'Ferry' | 6000 kwa siku |
| Meli Ndogo | 6000 kwa siku |
| Boti iliyobeba sanduku za kubeba samaki | 3000 kwa siku |
| Makontena | 6000 kwa siku |
| Mitumbwi ya kusafirisha abiria | 2,000/= kila safari |

USHURU WA MAEGESHO YA MAGARI YA BIASHARA KWENYE VITUO VYA KUTUA

| | |
|---|---|
| Gari lenye tani 1-3 | 1,000/= kwa siku |
| Gari lenye tani 4-7 | 1,500/= kwa siku |
| Gari lenye tani 7-10 | 2,000/= kwa siku |
| Gari la zaidi ya tani 10 | 5,000/= kwa siku |

SEHEMU YA TATU

MAOMBI YA KUCHIMBA/KUPITISHA MTARO KWENYE ENEO LA BARABARA

| | |
|---|---|
| Barabara za lami | Tsh 300,000/= |
| Barabara za kawaida | Tsh 100,000/= |

SEHEMU YA NNE

ADA NA USHURU WA MATANGAZO

Ada ya Mabango kwa mwaka

| | |
|---|---|
| Kila bango linalotoa mwanga litalipia | Tsh. 35,000/=kwa kila $M^2$ 1 kwa mwaka |
| Kila bango ambalo halitoi mwanga litalipia | Tsh 30,000/= kwa kila $M^2$ 1 kwa mwaka |

Ada ya Maombi ya kusimika mabango ya matangazo ya biashara

| | |
|---|---|
| 0.1 $M^2$ – 1$M^2$ | 2,000/= kwa kila ombi |
| 1.1 $M^2$ – 2$M^2$ | 4,000/= kwa kila ombi |
| 2.1 $M^2$ – 3$M^2$ | 6,000/= kwa kila ombi |
| 3.1 $M^2$ – 4$M^2$ | 8,000/= kwa kila ombi |
| 4.1 $M^2$ – 5$M^2$ | 10,000/= kwa kila ombi |
| 5.1 $M^2$ – nakuendelea | 25,000/= kwa kila ombi |
| Matangazo yaliyobandikwa kwenye ukuta/kuchorwa kwenye ukuta yatalipia | Tsh. 25,000/=kwa kila $M^2$ 1 kwa mwaka |

MATANGAZO YA BIASHARA 'PROMOTION'

| | |
|---|---|
| Matangazo ya biashara kwa wenyeji (ndani ya mkoa) | Tsh. 100,000/= kwa siku |
| Matangazo ya biashara kwa watu wanaotoka nje ya mkoa | Tsh. 150,000/= kwa siku |
| Kazi za sanaa kwa wasanii wa ndani ya mkoa | Tsh. 50,000/= kwa siku |
| Kazi za sanaa kwa wasanii wa nje ya mkoa | Tsh. 100,000/= kwasiku. |

SEHEMU YA TANO

ADA YA SUGHULI ZA UTAMADUNI

| Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|
| Kibali cha kusajili shughuli za utamaduni | Tsh 5000 kwa Mwaka |
| Kibali cha ngoma za jadi | Tsh.10,000/= kwa mwaka |
| Kibali cha kuchezesha disco, maonyesho ya bendi, sanaa za maonyesho (maigizo, mazigaombwe, sinema na video kwa vikundi vya ndani yaWilaya | Tsh. 30,000/=kwa mwaka |
| Kibali cha kuchezesha disco, maonyesho ya bendi, sanaa za maonyesho (maigizo, mazigaombwe, sinema na video kwa vikundi vya nje yaWilaya) | Tsh. 50,000/=kwa mwaka |
| Kibali cha kucheza michezo ya kubahatisha | Tsh. 30,000/= kwa kibali |
| Kibali cha mechi za mpira katika uwanja wa Halmashauri | 10% ya mapato kwa kila mechi |
| Ada ya kibali cha Tiba asili | Tsh. 30,000/= kwa mwaka |
| Ada ya kibali cha sherehe | Tsh 5,000/= kwa kila sherehe ya siku moja. |
| Ada ya kukodisha vyombo vya matangazo | Tshs 300,000/= kwa siku moja. |

SEHEMU YA SITA

USHURU WA KUCHINJA MIFUGO

| Mifugo | Machinjioni | Maeneo maalum (slaughter slub) kwa kila mfugo |
|---|---|---|
| Ng'ombe | 5,000/= | 3,000/= |
| Nguruwe | 5,000/= | 1,500/= |
| Mbuzi | 3,000/= | 1,500/= |
| Kondoo | 3,000/= | 1,500/= |
| Ngamia | 3,000/= | 1,500/= |
| | | |

*Tangazo la Serikali Na. 98 (linaendelea)*

ADA YA UKAGUZI WA WANYAMA (UKAGUZI WA AWALI MASAA 12 KABLA YA KUCHINJA):-

| Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|
| Ng'ombe | Tsh.500/= |
| Mbuzi/Kondoo | Tsh.300/= |
| Nguruwe | Tsh. 500/= |

ADA YA KUTUNZA NGOZI KWA MWEZI:-

| | |
|---|---|
| Ng'ombe, Mbuzi/Kondoo | Tsh.25,000/= |

ADA YA UKAGUZI WA NYAMA BAADA YA KUCHINJA:-

| | |
|---|---|
| Ng'ombe | Tsh. 1,000/= |
| Mbuzi/ Kondoo | Tsh. 500/= |
| Nguruwe | Tsh. 500/= |

SEHEMU YA SABA

ADA YA VIBALI VYA UJENZI

| ENEO LA SAKAFU LINALOZIDI META ZA ENEO ($M^2$) | ENEO LA SAKAFU LISILOZIDI META ZA ENEO ($M^2$) | VIWANGO VYA ADA |
|---|---|---|
| | 45.45 | 15,000/= |
| 45.45 | 92.01 | 20,000/= |
| 92.01 | 139.35 | 30,000/= |
| 139.35 | 185.81 | 45,000/= |
| 185.81 | 231.274 | 70,000/= |
| 231.274 | 278.71 | 50,000/= |

| | |
|---|---|
| Ongezeko la ada kwa kila meta moja ya mraba zaidi ya meta za mraba 278.71 | 150/= |
| Mabadiliko ya kuta za nje za jengo kwa upanuzi wowote | 31,600/= kima cha chini. |

---

JEDWALI LA PILI

---

KUFIFILISHA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 13)*

Mimi ………………………………………………wa S.L.P…………….……….. nakiri KWA HIYARI YANGU MWENYEWE mbele ya……………………………………..ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya ……………………………. kwamba mnamo tarehe……ya Mwezi….Mwaka………nilitenda kosa la kukiri masharti ya kifungu cha …………..cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya Musoma za mwaka 2017.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Niko tayari kulipa kiasi cha Ada na Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIYARI YANGU KWA KADIRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……………..ya mwezi……………mwaka……………………

Jina…………………………..…………………………...Saini……………………........

Mbele ya:

Jina…………………………..……………….<br>
Saini……………………………………..…........<br>
Wadhifa…………………………………………

Nembo na muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma umebadikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa Azimio lililopitishwa na Mkutano wa Baraza la Madiwani ulioitishwa tarehe 18 mwenzi Mei mwaka 2016 na ubandikwaji huo kushuhudiwa na:-

FLORA R. YONGOLO,<br>
*Mkurugenzi Mtendaji (W),*<br>
*Halmashauri ya Wilaya.*<br>
*Musoma*

CHARLES MAGOMA NYAMBITA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wiilaya,*
*Musoma*

NAKUBALI

Dodoma,
9 Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB.),
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tamisemi*